**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA**
**SHULE YA SEKONDARI MWANAMWEMA SHEIN**


**S. L. P 1601,**
**SINGIDA.**
**14/06/2023**

**<u>NAMBA ZA SIMU</u>**
MKUU WA SHULE**: 0759342391, 0788904608**
MAKAMU MKUU WA SHULE: **0759569510**

KUMB. NA.SDC. / MSSS/FV.JI/VOL.1 – 05
**MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI ……………………………………………….**
**S. L. P ………………………………………………………………..……………….…….**

**YAH. <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2023 KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWANAMWEMA SHEIN:</u>**

**1.** Ninafurahi kukuarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano Tahasusi ya HGK/HGL katika Shule ya Sekondari Mwanamwema Shein iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Mkoa wa Singida **HONGERA SANA**.

## <u>MAHALI ILIPO</u>

Shule ipo umbali wa km 27 mashariki mwa mji wa Singida barabara kuu iendayo Arusha na baada ya umbali wa km 15 kuna njia panda ya kuelekea Mgori km 12 **(kibao cha Shule kitakuelekeza)** Shule hii ni ya mchanganyiko, wavulana na wasichana kwa Kidato cha I hadi cha nne (IV) na kwa kidato cha tano na sita (V na VI) ni wasichana tu.

## <u>USAFIRI</u>

Usafiri wa kufika Shuleni ni wa Magari madogo ya abiria aina ya Noah ama Coaster wanafunzi wanaotoka nje ya Mkoa/Mji wa Singida, watashuka Stendi kuu ya mabasi Misuna, na kupanda bajaji au Bodadoda hadi blue Plaza (blue pharmacy) hapo utapanda Noah zinazoenda Mgori . Magari huondoka mjini Singida kati ya saa 7 mchana hadi saa 8 mchana tu. Ukifika Mgori, Shule ipo umbali wa km 0.5 kusini mwa stendi ya mabasi. Aidha siku za Jumamosi kuna usafiri mzuri wa kwenda Mgori na kurudi mjini Singida kuanzia saa 1;00 asubuhi mpaka saa 12 jioni, siku hiyo ya Jumamosi Noah zinahamia stand ndogo ya TRA, kimsingi eneo la TRA lipo karibu sana na BLUE PLAZA.

Muhula wa masomo utaanza **14/08/2023.** Hivyo Mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni **kuanzia 12/08/2023** kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saaa 12:00 jioni. Tafadhali hakikisha umefika shuleni kwa siku zilizotajwa vinginevyo unaweza kupoteza nafasi yako, ninasisitiza **MASOMO YANAANZA 14/08/2023**

Unapofika Shuleni hakikisha kuwa unaleta mahitaji yote yaliyoelekezwa na kuambatishwa na barua hii .

Aidha wanafunzi watakaokuwa wanalipiwa fedha ya michango na mamlaka mbalimbali za sehemu wanazotoka kwa mfumo serikali kuu, Halmashauri za Wilaya , Mji , Manispa, Jiji ,Vijiji au Wafadhili , Shule inaomba barua za mamlaka hizo zikielezea namna watakavyolipa na lini ili wasikwamishe uendeshaji wa shughuli za Shule.

## 2. MICHANGO YA KULIPA.

| AINA YA MCHANGO | KIASI | MAELEZO |
|---|---|---|
| Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000 | Kila mwaka |
| Fedha za tahadhari | 5,000 | mara moja (haitarejeshwa) |
| Kitambulisho | 5,000 | mara moja |
| Nembo ya shule | 5,000 | mara moja |
| **Jumla ya michango inayotakiwa kulipwa** | **80,000** | |

**NB.** Fedha hizi ziwekwe kwenye akaunti ya Shule Na. **50801100137** jina la Akaunti ni **MWANAMWEMA SHEIN SECONDARY SCHOOL**. Rec. Benki ya NMB .Original ya bank pay in slip ipelekwe kwa mhasibu wa **Shule (hakikisha bank pay in slip ina jina la mwanafunzi, kidato na orodha ya vitu ulivyolipia nyuma yake**.

**Angalizo: PESA ZOTE ZILIPWE BANK, ISIPOKUWA PESA YA TISHETI (15000) ZITAPOKELEWA SHULENI KAMA UTANUNUA SHULENI.**

## 3. SARE

### 3. 1 SARE YA SHULE

i Sketi 2 nyeusi kitambaa kizito cha suti **"grade one".** Sketi iwe ya marinda ya kupanga, 8 upande wa mbele na nyuma 8 jumla yawe marinda 16 mpaka kwenye jicho la mguu

ii Mashati 2 ya mikono mirefu meupe tetron nzito yasiyo na maua.

iii Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visivyo na visigino virefu.

iv Soksi ndefu nyeupe jozi mbili (**zinapatikana shule**)

**v** Sweta ya mikono mirefu RANGI YA KIJIVU aje nalo (**lakini pia linapatikana shule)**

vi Neck Tie Nyeusi au **(zinapatikana shule kwa shilingi 3,000/= )**

vii Wanafunzi wanaovaa hijab (kijuba) iwe nyeupe kitambaa aina ya HALUA na iwe ndefu kufika usawa wa nyonga.

viii Aje na T-shirt ya rangi ya **BLUE** ya kukolea au inapatikana karibu na shule kwa **Tshs 15,000/=**

**3.2 <u>NGUO / SARE ZA MICHEZO NA KAZI</u>**

i Bukta na T-shirt rangi ya bluu

ii Gauni moja au mbili mshono wa solo kitambaa cha **tetroni nzito drafti ndogo ya kijani na nyeupe** kwaajili ya kazi za nje na kushindia.

iii Wanafunzi wanaovaa **hijab (Kijuba) iwe ya rangi ya Damu ya mzee (Maroon) aina ya Halua na iwe ndefu kufika usawa wa nyonga**

iv Raba rangi yoyote ya kuvaa wakati wa michezo, kazi na wakati wa masomo ya jioni.

v Viatu aina ya simple/sandles vya kushindia (haruhusiwi kuvaa malapa)

vi Tracksuit ya bluu bahari na nguo za kulalia

**NB**: **Nguo za nyumbani haziruhusiwi (Atakayekuja na nguo isiyo sare ya shule atarudishwa nyumbani).**

- **Iwapo mwanafunzi ana changamoto ya kifua (Baridi) anaruhusiwa kuvaa Pull Neck nyeupe ndani ya shati la shule.**

**4. <u>MAHITAJI YA BWENI</u>**

(i) Shuka mbili rangi ya bluu bahari

(ii) Godoro la (unene) nchi 2 ½, urefu futi 6 na upana futi 3 **(Kwa mwenye changamoto ya usafiri,atakayehitaji Godoro awasiliane na uongozi wa shule kwa namba zilizopo juu ya fomu hii kwaajili ya kuweka oda ya Godoro**

(iii) Chandarua

(iv) Blanketi

(v) Taulo na nguo za ndani za kutosha.

(vi) Kitana, sabuni zakuogea na kufulia

(vii) Ndoo ya plastiki lita 10 au 20 kwa ajili ya kuogea na kufulia. **(Zinapatikana shule)**

(ix) Vifaa vya chakula (sahani, Bakuli, Kikombe na kijiko) **(Vinapatikana shule)**

(x) Sanduku gumu la chuma (tranka)

**5.1 <u>VIFAA VYA USAFI</u>**

- **KWA WANAFUNZI WA TAHASUSI YA HGL**

i Jembe jipya 1 na mpini wake

ii Reki

iii Fagio la chelewa **(VIFAA HIVI VYOTE VINAPATIKANA SHULE)**

iv Ndoo ya plastic lita 20

v Mopa

- **KWA WANAFUNZI WA TAHASUSI YA HGK**

i. Panga

ii. Fyekeo **(VIFAA HIVI VYOTE VINAPATIKANA SHULE)**

iii. Soft broom

iv. Ndoo ya plastic lita 20

v. Squeezer

**ANGALIZO**: **VIFAA HIVI VIKABIDHIWE SIKU YA KURIPOTI (SIO FEDHA) AKABIDHI VIFAA SIKU YA KURIPOTI KATIKA OFISI YA USAJILI**

**5.2 VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

i Daftari makubwa 8 ( counter books Q3 au Q4)

ii Rim 2 ya karatasi A4 (Zikabidhiwe Shuleni) **(Zinapatikana shule)**

iii Mathematical set (**Zinapatikana shule)**

iv Kalamu ya wino, Penseli na Ruler (**Zinapatikana shule)**

v Jalada (file) moja la kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi. (**Linapatikana shule)**

vi Bag kwaajili ya kubebea madaftari na vifaa vya darasani.

vii Vitabu vya tahasusi aliyopangiwa.

i. History – Author Walter Rodney.
Comrade Shibitali.
Bigirwamungu.

ii. Geography - Author Zisti Kamili.
D.T Msabila.
R.B Bunnet.
David Waugh

iii. Kiswahili – Tahakiki ya Kiswahili (Nyambari Nyangwine)
Nadharia ya fasihi kidato cha 5&6
Kiswahili 01 kidato cha 5&6 Oxford
Kamusi ya Kiswahili (TUKI)

iv. English language – Language 01 (Msabila)
Language 01 (Nicolous Asheri)
Advanced learner's Dictionary (Oxford)

NB: **KULINGANA NA MAZINGIRA YA SHULE KUWA MBALI NA MJI, NA ILI KURAHISISHA USAFIRI, VIFAA VIFUATAVYO VINAPATIKANA SHULE**

1. Soksi nyeupe
2. Sweta rangi ya kijivu
3. Neck Tie nyeusi
4. Fyekeo
5. Ndoo za plastiki lita 10 au 20
6. Vifaa vya chakula (Kontena, kikombe na kijiko)
7. Jembe na mpini wake
8. Reki
9. Fagio la chelewa
10. Mopa
11. Panga
13. Soft broom
14. Squeezer
15. Rim (karatasi nyeupe)
16. Mathematical sets
17. Kalamu ya wino
18. Penseli na Rula
19. Jalada (File)

**6 .<u>SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.</u>**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Raisi – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Hivyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

(**a**) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(**b**) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima

(**c**) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (kujisomea) ukiwa shuleni ama nyumbani

(**d**) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa

(**e**) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa mwanafunzi katika shule hii

(**f**) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(**g**) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(**h**) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na

(**i**) Kutunza mali za umma.

(**j**) Huruhusiwi kunyoa kipara, kufunga nywele ndefu,kufuga kucha ndefu ,kupaka rangi midomo na kucha ,kutinda nyusi, kupaka wanja , kuvaa heleni,bangili,mikufu,nguo fupi na nguo zisizo na heshima na adabu.

(**k**) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu au laini yoyote ya simu shuleni.

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.**

**(a)** Wizi

**(b)** Uasherati na Ushoga.

**(c)** Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, Cocaine, Mirungi, kuberi na kadhalika.

**(d)** Kupigana mwanafunzi kwa mwanafuzi, au mwanafunzi kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule

**(e)** Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

**(f)** Kudharau bendera ya Taifa .

**(g)** Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba.

**(h)** Kuolewa

**(i)** Kutoa mimba

**(j)** Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

**(k)** Kukataa adhabu kwa makusudi.

**(l)** Kumiliki, kukutwa au kutumia simu katika mazingira ya shule .

**(m)** Utoro wa kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa.

**(n)** Kulala nje ya shule Mwanafunzi wa Bweni (bila ruhusa)

**(o)** Kuwa bwenini muda wa masomo bila ruhusa.

**(p)** Kutohudhuri darasani, kujisomea wakati wa jioni (Preparation time)

**(q)** Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria

**(r)** Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla.

**(s)** Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kunywa sumu na n.k

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**MUHIMU: MWANAFUNZI ATAKAYE ONESHA UTOVU WOWOTE WA NIDHAMU SHULE HAITOSITA KUCHUKUA SHERIA AU TARATIBU ZILIZOWEKWA.**

**7. Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

**(a)** Medical Examination Forms ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara mwanafunzi atakapo ripoti Shuleni.

**(b)** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, na makosa ya jinai.

**(c)** Fomu ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**(d)** Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wanaoweza kuja kumtembelea shuleni na namba zao za simu

**(e)** Cheti halisi cha kuzaliwa na kivuli chake

**(f)** Nakala halisi ya matokeo ya kidato cha nne (statement of results) na kivuli chake

**8. Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU YA MWANAMWEMA HIGH SCHOOL**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI
MWANAMWEMA SHEIN
S.L.P 1601 SINGIDA
Tarehe: 14/06/2023 Sahihi:

**JUSTINA MUSSA CHINAMATA**

**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA**

**SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule:** 0759342391, 0788904608
- **Makamu Mkuu wa Shule:** 0759569510
- **Mwandamizi Taaluma:**0756604482
- **Mwandamizi Malezi :**0765734439

## FOMU YA MAPOKEZI

## FOMU HIZI ZIJAZWE NA KUREJESHWA NI MUHIMU KUKAMILISHA.

| **PICHA YA MWANAFUNZI** |
|---|

**(A) IJAZWE NA MWANAFUNZI**:

Mwanafunzi…………………………………………Taifa……………………………….

Raia……………………… Dini…………….Tarehe ya kuzaliwa…………………… Shule ya Sekondari uliyotoka……………………… Tarehe ya kutoka shule hiyo…………………saini ya Mwanafunzi………………………………………………Tarehe……………………….

| **PICHA YA MZAZI/MLEZI** |
|---|

**(B) IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

Jina la mzazi/mlezi……………………………………………Anuani kamili………………

**SEHEMU UNAPOISHI**:-Mtaa/kijiji………………………………… Jina la mwenyekiti wa serikali ya mtaa/Kijiji……………………Kata……………………Wilaya……………………

Mkoa……………… Namba ya nyumba…………Namba ya simu, ofisini au nyumbani ………………………………………..au jirani……………………………………….

**MAELEZO YA KIKAZI**: - Kazi ya Mzazi/Mlezi…………………………………….. Jina la Mwajiri……………………………………Idara………………………………………… Mahali ilipo…………………………………………………………Anuani ……………………………………………………….Namba ya simu…………………

Saini ya mzazi/Mlezi…………………………………Tarehe……………………….

**Taja ndugu watatu ambao wanaweza kutoa msaada au kumtembelea mwanao**

| No. | JINA KAMILI | KAZI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

**AHADI YA MZAZI/MLEZI:**

Mimi……………………………………………Mzazi/Mlezi wa…..……………………………
ambaye amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari ya Mwanamwema Shein mwaka **2023/2024**. Ninaahidi kulipa michango ya shule kwa wakati, Pia Nakiri kukubaliana na **sheria, kanuni** na **maelekezo** yaliyotolewa na shule ya sekondari ya Mwanamwema Shein, nimeyasoma na kuyaelewaa kikamilifu. Ninaahidi kuyasimamia ili mtoto wangu aya tekelezekwa ukamilifu.

Jina……………………………………………………………………………………….

Saini …………………………….. Tarehe ……………………………………………..

Namba ya Simu ……………………………………………………………….

**AHADI YA MWANAFUNZI:**

Mimi………………………………………………………………..mwanafunzi wa shule ya……………………………………………. ambaye nimechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari Mwanamwema Shein mwaka **2023/2024**. Nakiri kukubaliana na **sheria, kanuni** na **maelekezo** yaliyotolewa na shule ya sekondari Mwanamwema Shein, nimeyasoma na kuyaelewa kikamilifu na ninaahidi kusoma kwa bidii na kufaulu masomo yote.

Jina……………………………………………………………………………………..

Saini ……………………………………………………………………………

Tarehe … ………………………………Namba ya Simu ya mzazi/mlezi

# MWANAMWEMA SHEIN SECONDARY SCHOOL

## MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by medical officer in respect of all new students)

Full name ----------------------------------------------------------------------Age ------------------

1. Blood count (red and white) --------------------------------------------------------------------
2. Pregnancy test ----------------------------------------------------------------------------------
3. Urine examination ------------------------------------------------------------------------------
4. Stool examination ------------------------------------------------------------------------------
5. Syphilis -------------------------------------------------------------------------------------------
6. T.B Test ------------------------------------------------------------------------------------------
7. Ear test -------------------------------------------------------------------------------------------
8. Eye test -------------------------------------------------------------------------------------------
9. Spleen --------------------------------------------------------------------------------------------
10. Abdomen -----------------------------------------------------------------------------------------
11. Additional information or any other Physical, Mental, Hereditary of infectious diseases

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

-------------- Treatment after examination -----------------------------------------------------------------

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

**MEDICAL CERTIFICATE** I certificate that the above concerned has been examined and found fit into pursue for further education.

Signature ------------------------- Designation ---------------------------------------------------------

Station ---------------------------------------------------- (Official stamp) Date ---/----/20---

NB: **FOMU HII IJAZWE NA MGANGA KATIKA HOSPITALI INAYOTAMBULIKA NA SERIKALI**